Institute for International Criminal Investigations

NADIA's INITIATIVE

Foreign & Commonwealth Office

# USULI WA UTAFITI NA RASIMU YA KANUNI YA MAADILI YA KIMATAIFA KWA AJILI YA KUREKODI NA KUCHUNGUZA UKATILI WA KINGONO UNAOHUSIANA NA MGOGORO ("KANUNI YA MAADILI YA MURAD")

*JUNI 2020*

1. Utafiti huu unajumuisha rasimu ya kanuni ya maadili ya kimataifa kwa ajili ya kurekodi na kuchunguza ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro.[1] Rasimu ya kanuni ya maadili imeambatishwa kwenye Kiambatisho A. Rasimu ya kanuni ya maadili imepewa jina la malenga wa ushairi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, Nadia Murad, jina ambalo linaakisi lengo la kutanguliza haki za wahanga. Utafiti huu pia unaonesha wa maendeleo ya rasimu ya kanuni ya maadili na inaelezea mchakato wa mashauriano ya kimataifa kuhusu Kanuni hiyo ya Maadili.
2. Wazo la kanuni hiyo ya maadili lilianzishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Uhalifu wa Kimataifa (IICI). Mradi wa kutengeneza Kanuni hii ya maadili ni ushirikiano kati ya IICI na Mradi wa Kuzuia Ukatili wa Kingono katika Mgogoro (PSVI)
3. Kutengeneza rasimu ya Kanuni ya Maadili kwa ajili ya mashauriano ya kimataifa, ya wazi, kumekuwa na mchakato mkubwa wa utafiti linganishi na majadiliano ya awali au "mahojiano" pamoja na watendaji na wadau 166. Rasimu ya Kanuni ya Maadili itazinduliwa rasmi kwa ajili ya mashauriano ya kimataifa ndani ya miezi ijayo. Majadiliano hayo na mchakato wa muda mrefu ili kutekeleza Kanuni iliyokamilika kutahusisha watendaji na wadau kutoka duniani kote.
4. Malengo yanayohusiana ya Kanuni ya Maadili ya Murad na mchakato unaohusika ni:
   - (a) Kuchuja viwango vya kuanzia au vya msingi vilivyopo (badala ya kutengeneza vipya ambavyo ni muhimu sana kwa ajili ya kurekodi kwa njia salama, fanisi na inayomlenga mhanga wa ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro kupitia utengenezaji na utekelezaji wa kanuni ya maadili inayoungwa mkono kimataifa.[2]
   - (b) Kuhusiana na michakato ya kurekodi, kuimarisha heshima, na utimizaji wa haki za binadamu za mhanga na shahidi, ikiwa ni pamoja na kuhusiana na utu, faragha, afya, usalama, ustawi, haki, tiba na maendeleo.
   - (c) Kuzuia madhara zaidi, ikiwa ni pamoja na kupewa kiwewe tena, walichosababishiwa wahanga.
   - (d) Kwa ujumla, kuimarisha ufanisi wa jitihada hizi za kuandika kumbukumbu, hivyo kuimarisha uwezekano wa matokeo bora zaidi kwa ajili ya wahanga, na, hatimaye, kwa wale wanaoandika kumbukumbu na jumuiya pana za mahali husika, kitaifa na kimataifa.

[1] Kwa kusudi la utafiti huu na rasimu ya kanuni ya maadili ya Murad, "ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro" hurejelea ukatili wa kingono kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya binadamu, kitendo cha mauaji ya kimbari au ukuiukaji mwingine mkubwa wa sheria ya kimataifa ya uhalifu wa kimataifa na haki za binadamu. Fasili hii ni pana na inajumuisha fasili ya "ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro na uovu" inayotumika katika *Itifaki ya Kimataifa juu ya Uandikaji wa Kumbukumbu na Uchunguzi wa Ukatili wa Kingono katika Mgogoro* (toleo la 2, 2017), uk, 11. Fasili hii inatumika kwa sababu za kiutendaji na kuakisi kwa sehemu kiini cha Hatua ya Kanuni ya Maadili ya Murad katika *Itifaki ya Kimataifa* iliyotajwa; haijakusudiwa kuzuia matumizi yanayoweza kutokea au umuhimu wa Kanuni ya Maadili ya Murad.

[2] Kiambatisho B kinajumuisha mifano ya vyanzo vya utafiti vilivyotumiwa katika maandalizi ya utengenezaji wa rasimu ya Kanuni ya Maadili ya Murad.

(e) Kuweka mifumo ya usaidizi na kutoa mwongozo tendaji wa kuhakikisha watendaji wote wanaweza kujizatiti na kufuata Kanuni hii ya Maadili, katika majukumu yao, bila kutengeneza vikwazo vyovyote visivyoondoleka kwa wale ambao wako tayari na wanaweza kufanya kazi kwa maslahi mapana ya wahanga.

## A. Kanuni hii ya Maadili inalenga kushughulikia tatizo gani?

5. Wale ambao wanaandika kumbukumbu, kuchunguza, kufuatilia kufanya utafiti na kutoa ripoti ("kuandika kumbukumbu") kuhusu ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro wanapaswa kuongozwa na sheria iliyopo, viwango vya kuanzia na namna bora ya utekelezaji kuhusu namna nzuri ya kuandika kumbukumbu hizo. Hii hujumuisha kuandika kumbukumbu kwa ajili ya utetezi, ufuatailiaji na kutoa ripoti kuhusu haki za binadamu, utafutaji ukweli, haki ya mpito, maamuzi ya mahakama za kiraia, kufungua madai kimkakati, madai ya hifadhi na makusudi ya haki ya makosa ya uhalifu. Kuna machapisho kadhaa ya kiufundi kutoka katika sekta mbalimbali ambayo yanaangazia mwongozo huo na namna bora ya utekelezaji. Yanajumuisha *Itifaki ya Kimataifa kuhusu Uandikaji Kumbukumbu na Uchunguzi wa Ukatili wa Kijinsia katika Mgogoro (2017).* Hata hivyo, kuna ripoti zinazoongezeka ambazo baadhi ya watendaji, kuanzia bodi za kitaifa na za kimataifa za uandikaji kumbukumbu hadi Mashirikia Yasiyo ya Kiserikiali (NGO) na wafadhili, hawajui au hawatumii miongozo iliyopo.

6. Sababu ya kushindwa huko hujumuisha kwamba waandikaji kumbkumbu, wachunguzi na watendaji wengine:

   (a) wanaona mwongozo huo ni mrefu sana au ni mgumu sana kuutumia, mara nyingi katika mazingira ambayo rasilimali ni chache, au wanaona vigumu kubainisha viwango vya kuanzia au vya msingi kutoka miongoni mwa mingozo mingi;

   (b) kwa kukosea, lakini kwa nia njema, wanaweka mkazo kwenye idadi ya wahanga waliohojiwa au wanahitaji kupata ushuhuda kwa haraka badala ya kupaswa kufuata vitendo vya kimaadili, salama na vyenye ufanisi ambavyo huheshimu haki na maslahi ya mhanga, ikiwa ni pamoja na haki na maslahi mapana ya watoto;

   (c) hufanya kazi kwa kujitenga, bila kushirikiana na watendaji wengineo, wanawahoji wahanga kwa kurudiarudia, kwa mahojiano yasiyo ya lazima na ambayo mara nyingi yanaweza kusababisha kiwewe tena.

   (d) wanaweka kipeumbele kwenye mahojiano na wahanga kimakosa wakati vyanzo mbadala vya taarifa vinaweza kutosha; au

   (e) wanaweka kipaumbele kufikia malengo yao binafsi badala ya kuheshimu haki na matamanio ya wahanga, ikiwa ni pamoja na mhanga kupata tiba yenye ufanisi na kupata haki (ikiwa haki ndilo hitaji lao).

7. Wahanga wameelezea baadhi ya matatizo kulingana na vile wanavyoona. Watendaji pia wamebainisha matatizo kuhusiana na usalama, matumizi na ufanisi wa kurekodi. Matatizo hayo hujumuisha:

   (a) mahojiano ya kujirudia na yasiyo ya lazima kwa whanga wa ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro bila kujaribu au kujaribu kidogo kuratibu au kuepuka kufanya mahojiano tena;

   (b) mahojiano yamefanywa na mtu ambaye hana mafunzo au asiye na ujuzi kwa kutumia mbnu za haraka, zisizo na ufanisi, zisizo salama au vinginevyo njia za hatari au kutozingatia muktadha, yote hayo yanaweza yasifanikiwe kufikia lengo ambalo kwalo mhanga ametoa taarifa zake;

   (c) waandika kumbukumbu hawajui kuhusu njia ambazo kwazo mbinu hizo zinaweza kusababisha madhara au kuwapatia tena kiwewe wahanga;

   (d) taratibu za kuomba idhini zisizojitosheleza au zenye msukumo mkubwa ambazo hazimpatii mhanga maelezo kamili ya machaguo na hatari, au muda na nafasi ya kufanya machanguzi yao wenyewe, na wahanga kutopokea majibu ya matokeo kama walivyoahidiwa;

   (e) ukosefu wa usaidizi wa matibabu na saikolojia ya kijamii ambao wahanga huenda wakauhitaji kufuatia uzoefu wao au kwa sababu ya athari za mahojiano yanayosababisha kiwewe tena; na

(f) mipango hafifu kuhusiana na ulinzi na hatari nyinginezo na miktadha ya mahali husika, ikiwa ni pamoja na kukutana na wahanga katika maeneo ambapo mahojiano yanaweza kushuhudiwa, kusikilizwa au kuingiliwa na wengine.

8. Vitendo vya kuandika kumbukumbu ambavyo si fanisi, si salama au si vya kimaadili, viwe na nia njema kwa namna yoyote ile, kusababisha au kuzidisha madhara waliyoyapata wahanga. Huharibu uwezekano wao wa kupata haki (mfano, ikiwa mahojiano yaliyorudiwa yatasababisha kumbukumbu zisizo linganifu au zisizo sahihi. Huhafifisha heshima ya haki za binadamu nyinginezo za wahanga na huenda ikahafifisha imani yao kwa utawala wa sheria na mifumo mingineyo ya utawala na kushughulikia migogoro. Vitendo vya kuandika kumbukumbu ambavyo vinahafifisha viwango hivyo vya kuanzia ni nadra sana kuwa na ufanisi na haviongezi thamani kwa kile ambacho kiliahidiwa kwa wahanga.

## B. Kanuni ya Maadili ya Murad inaweza kusaidiaje?

9. Ni kwa jisni gani watendaji na wadau wanaweza kuhimiza kwa ufanisi na kusaidia jumuiya kuhusu namna bora ya kuandika kumbukumbu na kufanya uchunguzi duniani kote? Tunaweza kuhakikisha vipi kuwa uandikaji wa kumbukumbu unafanyika pale ambapo ni lazima tu na ndicho kitu ambacho wahanga wanakitaka? Kwamba kazi ipi ambayo ni salama, yenye ufanisi, inayomlenga mhanga na huheshimu haki na malengo ya wahanga? Je, tunaweza kuhakikishaje kwamba uandikaji kumbukumbu unaheshimu majukumu ya watendaji wengine wanaofanya kazi na wahanga? Suluhisho linaweza kuwa ni kanuni ya maadili ya kimataifa, ikizingatiwa na kutekelezwa na serikali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika mengineyo yanayoshirikiana na serikali, polisi, mamlaka mengineyo ya uchunguzi ya kitaifa na kimataifa, mashirika ya kiraia na wafadhili; kanuni ya maadili ambayo inatumika bila kujali ni nani anayeshughulika, kusimamia, kuomba au anatoa fedha au anatumia watu wengine kuchukua hizo kumbukumbu, au yule ambaye anatumia taarifa au ushahidi uliokusanywa na wengine.

10. Kanuni ya maadili inayoungwa mkono kimataifa, yenyewe tu haitaweza kuimarisha hali kwa muda mfupi tu. Utakuwa ni mchakato unaohusisha tathmini binafsi, mazungumzo, mafunzo na usaidizi wa pamoja, na ushirikiano katika sekta zote na baina ya wahanga, watendaji na wadau. Itahitaji mapitio ya mbinu, sera na taratibu zilizopo. Itahitaji jitihada za pamoja kadri ya muda unavyokwenda, uondoaji wa vichocheo vya uandikaji wa kumbukumbu usiokuwa na ufanisi, na uimarishaji wa motisha kwa kazi inayomlenga mhanga. Kwa ufupi, itahitaji urekebishaji tena wa mfumo wa ikolojia ambao kwa huo hufanyika uandikaji wa kumbukumbu ya ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro.

11. Wakati wa mazungumzo ya awali kati ya Julai 2019 hadi Februari 2020 takribani wahanga 166, watendaji na wadau kutoka sekta na maeneo mbalimbali walionesha kuunga mkono kanuni hiyo ya maadili kuwa ni mchango mzuri wa kushughulikia matatizo yaliyoainishwa na kufikia malengo yaliyowekwa katika aya ya 4.

## C. Tangazo na hati ya mhanga

12. Rasimu ya mwisho ya kanuni ya maadili itaambatana na tangazo lililoandaliwa na IICI, pamoja na hati ya mhanga, ili kusaidia matumizi ya kanuni hiyo ya maadili katika miktadha mbalimbali.[3]

13. Tangazo litaunganisha mazingatio ya msingi ya Kanuni ya Maadili na nyenzo muhimu, miongozo, marejeo na vyanzo vya sheria ya kimataifa. Tangazo pia litajumuisha njia jumuishi za kujifunza na utekelezaji, na za kiubunifu ili kutumia Kanuni hii ya Maadili katika sekta na miktadha yote, na ndani ya aina tofauti za uhaba wa rasilimali na uhalisia.

[3] Wakati tangazo na hati ya mhanga zinaweza kuwa nyaraka muhimu saidizi, makubaliano ya kuunga mkono Kanuni ya Maadili ya Murad yenyewe tu hayawezi kujumuisha makubaliano ya tangazo na hati ya mhanga.

14. Wahanga wataonekana kwenye hati ya mhanga, wakionesha mitazamo yao. Hati hii itawasaidia waandika kumbukumbu kuelewa kile ambacho wahanga wanahitaji na kutaka uandikaji wa kumbukumbu na kujihusisha nao. Itawasaidia waandika kumbukumbu na wachunguzi kuelewa vizuri na kutumia Kanuni ya Maadili.

## D. Mchakato na mbinu za kuwezesha kuzindua rasimu ya Kanuni ya Murad

15. Awamu ya 1 ilihusisha *utafiti* linganifu katika maeneo tofautitofauti na kutathimini kanuni za maadili zilizopo, njia bora za utekelezaji na miongozo inayohusiana na uandikaji wa kumbukumbu wa ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro. Hii ilikuwa inakusudia kutathmini viwango vya msingi na kuwa na uelewa kutoka katika makundi yote yanayojihusisha na wahanga. Mifano ya vyanzo vilivyotumiwa imewekwa katika Kiambatisho B.

16. Awamu ya 2 ilihusisha kufanya *mahojiano* ya ana kwa ana, kwa njia ya masafa na kwa maandishi kutoka kwa watendaji, wahanga na wadau kuhusu dhana ya kanuni ya maadili ya kimataifa na kuhusu viwango vya msingi vinavyopaswa kujumuishwa. Awamu hii ilifanyika kuanzia Julai 2019 hadi Februari 2020. Maswali kadhaa ya kawaida yalitumika kuongoza mahojiano, yakiwa yamejikita katika kujua viwango hivyo vinaweza kuwa vya aina gani, na vinapaswa kutumika kwa nani. Mahojiano mengi yalidumu kati ya dakika 90-80.

17. Watu mia moja na sitini na sita walihusishawa. Walijumuisha wahanga ambao walishiriki katika mchakato wa kuandika kumbukumbu na wataalamu wa kujitegemea. Washiriki wengi walikuwa wanahusiana na (a) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) ya kitaifa na kimataifa; (b) mashirika na ofisi za Umoja wa Mataifa; (c) mamlaka ya uchunguzi na kuendesha mashtaka ya kitaifa na kimataifa au mashirika yanayowezesha uandikaji huo wa kumbukumbu; (d) watendaji wa mashirika ya kiraia yasiyo ya kiserikali ya kimataifa; (e) serikali; (f) wataalamu wa afya na wanasheria; (g) wanataaluma, ikiwa ni pamoja na wale waliobobea katika utafiti wa ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro na vyombo vya habari vinavyoripoti na maadili ya kazi hiyo; na (h) wafadhili ambao ni serikali na wale ambao si serikali. Mahojiano yalifanywa kutoka kwa watu ambao wanatoka au wanafanya kazi katika nchi mbalimbali duniani, kuanzia Peru, Argentina, Colombia, Mexico, Marekani, Indonesia, Bangladesh, Myanmar, Sri Lanka, Iraki na Siria hadi Chadi, Uganda, Kenya, Sudani Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Gambia, Afrika Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Uswisi.

18. Mahojiano hadi leo yamelenga kuwa wakilishi kadri iwezekanavyo. Hata hivyo, zilikuwa ni hatua za awali tu ili kuhakikisha rasimu ya kanuni ya maadili inajumuisha maoni na uzoefu mbalimbali. IIC inakiri kuwepo kwa mapengo kadhaa; kwa mfano, matarajio yalikuwa ni kufanya mahojiano mengi zaidi kutoka kwa wahanga na kutoka kwa wachunguzi wa kitaifa na mamlaka yenye uwezo wa kuchunguza. Mashauriano ya kimataifa ambayo yatafuatia baada ya uzinduzi wa rasimu ya Kanuni ya Maaadili ya Murad yatahusisha ushiriki na ujumuishaji mpana na utatafuta kuziba mapengo katika uhusikaji hadi sasa.

19. Awamu ya 3 ilihusiha *maandalizi ya rasimu ya kanuni ya maadili ya Murad.* Iliandikwa mwezi Februari 2020 kulingana na utafiti na mahojiano.

## E. Nini kinachofuatia? *[Baadhi ya hatua zinazofuata huenda zikabadilishwa kwa sababu ya athari ya virusi vya korona]*

20. **Uzinduzi wa rasimu ya Kanuni ya Maadili ya Murad:** Mchakato wa Kanuni ya Maadili ya Murad utazinduliwa rasmi na rasimu ya Kanuni ya maadili kuwasilishwa kwa ajili ya mashauriano ya kimataifa na uendelezaji zaidi katika nusu ya mwaka 2020. Itawekwa katika tovuti ya Kanuni ya Maadili ya Murad, ambapo maoni kuhusu rasimu ya kanuni ya Maadili yatawasilishwa. Wahanga, serikali, watendaji na mashirika kutoka katika sekta mbalimbali na duniani watahimizwa kujihusisha na rasimu ya Kanuni ya Maadili na kusaidia kujenga maafikiano juu ya Kanuni ya Maadili yenye nguvu ambayo ina uungwaji mkono mkubwa

21. Baada ya uzinduzi wa rasimu ya Kanuni ya Maadili: *Mashauriano ya kimataifa,* kwa maandishi, ana kwa ana na kwa njia ya masafa kuhusu rasimu ya Kanuni ya Maadili yatalenga kuwahusisha na kupokea maoni kuhusu

rasimu ya Kanuni ya Maadili kutoka kwa watendaji wengi, sekta na maeneo kadri iwezekanavyo. Wakati wa mashauriano, mifano halisi zaidi ya jinsi ya kutumia viwango vya msingi katika miktadha yenye changamoto itakusanywa ili kuimarisha tangazo linalounga mkono Kanuni ya Maadili. Mahojiano pia yalibainishwa lakini yameachwa wazi kwa ajili ya majadiliano zaidi kuhusu maswali muhimu yanayohusu mkazo, ufikiaji na uchukuaji wa rasimu ya mwisho ya Kanuni ya Maadili ya Murad, na haya yatatolewa kama maswali ya msingi wakati wa mashauriano ya kimataifa (tazama aya ya 27). Mashauriano pia yatashughulikia hitaji, wajibu na mambo mengine mahususi ya utekelezaji au mfumo utakaowezesha Kanuni ya Maadili.

22. Mara baada ya mashauriano ya kimataifa kukamilika na rasimu ya Kanuni ya Maadili imehakikiwa ili kuonesha matokeo ya mashauriano ya kimataifa, *rasimu ya mwisho ya Kanuni ya Maadili ya Murad* itazinduliwa mapema mwaka 2021. Hii itaambatana na tangazo na hati ya mhanga kama ilivyoelezwa katika aya za 12-14. Tangazo litakuwa nyaraka hai (inayoweza kufanyiwa marekebisho mara kwa mara).

23. Zana za utekelezaji kwa ajili ya sekta mahususi zitatengenezwa kwa kushirikiana na watendaji na wadau (kwa mfano, kwa kushirikiana na wafadhili, zana/mwongozo wa utekelezaji wa Kanuni ya Maadili iliyotengenezwa kwa ajili ya mahitaji yao).

## F. Taarifa zaidi kuhusu Kanuni ya Maadili ya Murad, istilahi yake na masuala kwa ajili ya mashauriano ya kimataifa

24. Rasimu ya kanuni ya maadili inapata hamasa na maudhui yake kutokana na matokeo ya utafiti na mahojiano ya kina na wahanga na watendaji. Inatafuta kuweka bayana viwango vya msingi vilivyopo, utaratibu wa msingi wa uandikaji kumbukumbu na viwango vya uchunguzi. Inatafuta kuweka, katika muundo wa kanuni na mazingatio, viwango vya msingi vinavyotumika bila kujali mazingira na rasilimali. Watendaji kadhaa walikubali kwamba ni jambo la bahati mbaya lakini la lazima kwa kanuni hiyo kujikita katika viwango vya kuanzia badala ya viwango vya juu kabisa au vinavyotamaniwa.

25. Rasimu ya Kanuni ya Maadili iliandikwa kama msingi wa kuendeleza majadiliano ya kina na mashauriano ya kimataifa. Inaweza kufupishwa au kuongezwa. Rasimu ya mwisho ya kanuni inaweza isiondoe uandikaji wa kumbukumbu na miongozo ya uchunguzi ya kiufundi au mahususi kwa ajili ya sekta wenye urefu na maelezo ya kina. Haitafanya kazi husika na ambayo ni ngumu ya uandikaji wa kumbukumbu na uchunguzi kuwa rahisi mara moja. Hata hivyo, itasaidia kubainisha kanuni za msingi na viwango, mistari miekundu isiyoruhusu majadiliano, ambayo miongozo mingi iliyopo haielezei kwa uwazi.

26. Kwa sehemu inaakisi mianzo yake kwenye PSVI na (*Itifaki ya Kimataifa kuhusu Uandikaji wa Kumbukumbu na Uchunguzi wa Ukatili wa Kingono katika Mgogoro* (2017), rasimu ya sasa ya Kanuni ya maadili inajikita katika:

(a) Ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro unaofasiliwa kama ukatili wa kingono ambao hujumuisha uhalifu wa kimataifa wa mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya binadamu au uhalifu wa kivita na ukiukaji mwingineo wa kimfumo wa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu.[4]

(b) Uandikaji wa kumbukumbu na uchunguzi kwa ajili ya haki, michakato ambayo inaweza kuhusiana na upatikanaji haki. Kwa mfano, inaweza kujumuisha waandishi wa habari, watu maarufu, wanasiasa na watendaji wengineo ambao si wachunguzi, lakini ambao wakati mwingine wanajihusisha na wahanga wa ukatili wa kingono unaohuisiana na mgogoro kwa njia ambazo zingekuwa muhimu katika michakato ya kutafuta haki inayofuata baadaye. (Kwa mfano, rekodi ya video ya mkutano kati ya mwandishi wa habari au mwanadiplomasia mwenye hadhi ya juu na mhanga, baadaye inaweza kutumiwa katika tume ya maulizo ya Umoja wa Mataifa, ripoti ya Shirika Lisilo la Kiserikali linalotetea haki za binadamu, programu ya fidia au kesi ya mahakama.) Rasimu ya Kanuni ya Maadili pia inakusudia kuwajumuisha wale ambao wanaomba, kuripoti, kuwezesha, kufadhili au wanatafuta kutegemea kazi hiyo.

[4] Tazama kijachini namba 1 kuona asili ya fasili hii. Hujumuisha ukatili uliofanywa na watendaji ambao si dola.

(c) "Haki (kutenda kwa haki)", imetumika kwa mapana kadri iwezekanavyo ili kujumuisha na kuamsha aina zote za haki, kama vile utambuaji wa haki, kusema ukweli, hati ya maombi, fidia, tiba zenye ufanisi, kutambua au kuwa na uelewa wa uhalifu na ukiukwaji, michakato ya mahakama rasmi ya kiraia au uhalifu, vile vile aina nyingine zaidi zisizo rasmi au za kitamaduni za kutenda haki. Haki humaanisha mambo tofauti katika nyakati tofauti kwa watu tofauti, ikiwa ni pamoja na wahanga wenyewe. Kanuni hii ya maadili haichukuliwi kwamba kutenda haki kuna umuhimu mahususi kwa wahanga wote; badala yake, inatafuta kuhimiza uelewa wa haki ambao unajumuisha dhana zinazofasiliwa na mhanga wa haki na mahitaji na malengo mengineyo ya wahanga.

(d) "Uandikaji wa Kumbukumbu" na "uchunguzi", katika maana ya kukusanya na kuweka kumbukumbu ya mambo kutoka kwa na kuwahusu wahanga na mashahidi kuhusu ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro kwa ajili ya matumizi mengine tofauti na uponyaji na huduma yao ya moja kwa moja.

27. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa awali, maudhui ya mwisho na hadhira lengwa ya rasimu ya Kanuni ya maadili inabaki miongoni mwa maswali muhimu yaliyo wazi kwa ajili ya mashauriano ya kimataifa. Mifano ya maswali mengine muhimu yaliyowazi ni:

(a) Je, Kanuni hii ya maadili inapaswa kujikita zaidi katika uandikaji wa kumbukumbu na uchunguzi kwa ajili ya aina mbalimbali za makusudi ya haki? [5]

(b) Je, kanuni hii inapaswa kujikita katika ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro, au inapaswa ijumuishe ukatili wa kijinsia unaohusiana na migogoro na ukiukaji na uhalifu usiokuwa wa SGBV? [6]

(c) Je, (rasimu ya) Kanuni ya Maadili imezingatia mitazamo tofauti na maamuzi ya aina mbalimbali za watendaji, kuanzia polisi wa kitaifa hadi vyombo na wafadhili wa kimataifa?

(d) Je, Kanuni ya maadili ishughulikia maswali yanayohusu uwajibikaji wa watendaji ambao wanashindwa kuheshimu haki za wahanga na kwa nyongeza, Kanuni ya Maadili, na ya kuanzisha, kama mhanga alivyoomba, mianya ya maoni au malalamiko kuhusu utendaji wa watendaji waliohusika katika uandikaji wa kumbukumbu na uchunguzi wa ukatili wa kingono unaohusiana na mgogoro?

(e) Je, kuna vipengele vya rasimu ya Kanuni ya Maadili ambayo haiakisi haki za mhanga, au vinginevyo inaweza kuwa tatizo au ina athari ambazo hazikukusudiwa? [7]

28. Rasimu ya kanuni ya maadili inapendekezwa kama mjumuiko wa maadili ya msingi, viwango, kanuni na njia za utekelezaji zinazolenga kupunguza madhara na kuboresha matokeo kwa wahanga. Sekta na tasinia nyingi wataona kanuni zilizopo katika rasimu ya Kanuni ya maadili zinafahamika, kwa kuwa zimetengenezwa kwa kuzingatia haki za mhanga na maadili ya msingi ya kawaida katika sekta zote na miongozo ya tasnia, itifaki na miongozo ya kiufundi. Kwa kutegemea matokeo ya mashauriano ya kimataifa, inatarajiwa kwamba rasimu ya

[5] Mahojiano kadhaa yalijikita katika uungaji mkono wa mawanda mapana, yakidai kwamba kutokana na mtazamo wa mhanga kuna viwango vya kuanzia ambavyo vinatumika bila kujali ni nani anayekutana nao ili kuchukua visa vyao, ama wale wanaokutana nao ni waandishi wa habari, watoa misaada ya kibinadamu, viongozi wa hadhi ya juu kutoka katika dola au shirika kubwa la kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa, watu maarufu, watafiti wa kitaaluma, watatezi wa haki za binadamu, wasimamizi au wachunguzi, au wachunguzi wa uhalifu.

[6] Majadiliano kadhaa yalipendekeza mtazamo mpana ili: kutafakari kwamba wahanga wengi wa ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro wa kingono pia ni wahanga wa uhalifu mwingineo na kwamba ukatili wa kingono unahusishwa na au ni sehemu ya ukiukaji na uhalifu mwingineo; kuepuka kuimarisha uzingatiaji wa jumuiya ya kimataifa kwenye ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro kuondoa uhalifu wa kijinsia unaohusiana na migogoro, SGBV wakati wa amani na uhalifu na ukiukaji usiokuwa wa SGBV; na kutambua kwamba wahanga wa uhalifu na ukiukaji mwingineo wana haki zile zile

[7] Kwa mfano, tafiti za kisayansi na uozefu wa kitaaluma unaonyesha kwamba uandikaji wa kumbukumbu na uchunguzi wa ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro unaweza kufanywa katika muktadha wa kundi (yaani, kwa waandika kumbukumbu kukutana na kundi la wahanga) bila kusababisha au kuchochea madhara kwa wahanga na bila kuharibu umuhimu na uaminikaji wa ushahidi, ikiwa ni pamoja na kuhusiana na taarifa ambayo waandika kumbukumbu wanaweza kutaka kuwasilisha kama ushahidi mahakamani na majukwaa mengineyo ya haki za binadamu? Ikiwa ndivyo hivyo, je, rasimu ya Kanuni ya Maadili inatosheleza kuruhusu ushiriki huo wa kundi?

mwisho ya Kanuni ya Maadili inaweza kutumika kama lugha ya msingi majumui na seti ya mazingatio katika sekta na miktadha yote.

29. Ikiwa mashauriano ya kimataifa yataamua kujikita katika mambo mahususi, utangulizi wa rasimu ya mwisho unaweza kujumuisha kauli itakayokuwa inaonyesha kwamba viwango vya msingi vya Kanuni ya Maadili huenda vikatumika na vina manufaa zaidi ya vipengele vya rasimu ya mwisho ya Kanuni ya Maadli, na kwamba hakuna kitu kwenye Kanuni hiyo ya maadili ambacho kinaweza kupendekeza kwamba viwango rahisi vinatumika zaidi ya mipaka yake iliyokubaliwa au kwa wahanga wa uhalifu au ukiukaji mwingineo.

**KIAMBATISHO A: RASIMU YA KANUNI YA MAADILI YA MURAD KWA AJILI YA MASHAURIANO YA KIMATAIFA NA UENDELEZAJI ZAIDI**

*Rasimu hii ya Kanuni ya Maadili inapaswa kusomwa pamoja na usuli wa utafiti ambao ni sehemu yake.*

## RASIMU YA KANUNI YA MAADILI YA KIMATAIFA KWA AJILI YA UCHUNGUZI NA UANDIKAJI WA KUMBUKUMBU WA UKATILI WA KINGONO UNAOHUSIANA NA MIGOGORO[1]

Kusudi la kanuni hii ya maadili ni kujenga na kuisaidia jumuiya juu ya njia bora ya utendaji ambayo ni salama, ya kimaadili zaidi na yenye ufanisi zaidi ambayo inafuata sheria za kimataifa. Ni kwa wale ambao wanakutana moja kwa moja na wahanga (kama vile wachnguzi, waandikaji wa kumbukumbu, waandishi wa habari, watafiti, viongozi wa hadhi ya juu, watu maarufu, wakalimani, wasuluhishi) na wale ambao wanaweza kushawishi mazinbgira ambamo maingiliano pamoja na wahanga yanafanyika (kama vile watunga sera, wanasiasa, wafadhili, viongozi wa mashirika, wabunifu na mameneja mradi, na wapokeaji wa kazi).

| KANUNI NANE ZA MSINGI | | | |
|---|---|---|---|
| MHANGA KWANZA | CHUKUA MUDA, SUBIRI KWANZA | MAARIFA NA UELEWA WA MAHALI HUSIKA | MAANDALIZI KAMA MSINGI |
| ONGEZA THAMANI AU USIFANYE | MIFUMO, UMAHIRI NA UENDELEZAJI | MAHOJIAONO YA HESHIMA NA SALAMA | UADILIFU NA UWAJIBIKAJI |

Kwa kuzingatia kushikilia Kanuni hii ya Maadili, tunajizatiti kufanya utekelezaji ulio salama, wa kimaadili na wenye ufanisi ili kusaidia haki za wahanga, na kujenga jumuiya inayofanya mambo ambayo yanadumisha na kukuza Kanuni hii ya Maadili. Tunatambua kwamba kila Kanuni na Mazingatio ya Kanuni ya Maadili yanategemeana na kuhusiana na yanatumika katika mitadha yote.

### 1. MHANGA KWANZA

1.1 **Mbinu Inayomlenga Mtu Binafsi:** Tutashughulika na wahanga kama mtu mmoja wa kipekee. Tutaiandaa mbinu yetu kwa haki, mahitaji, matamanio na hatari ambayo ni mahususi kwa mhanga husika, tukitambua uwezo wake mbalimbali, changamoto na uhatari kulingana na ni akina nani na sehemu walipo. Tunatambua kwamba kuelewa

[1] Kwa kusudi la utafiti huu na rasimu ya kanuni ya maadili ya Murad, "ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro" hurejelea ukatili wa kingono kama uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya binadamu, kitendo cha mauaji ya kimbari au ukuiukaji mwingine mkubwa wa sheria ya kimataifa ya uhalifu wa kimataifa na haki za binadamu. Fasili hii ni pana na inajumuisha fasili ya "ukatili wa kingono unaohusiana na migogoro na uovu" inayotumika katika *Itifaki ya Kimataifa juu ya Uandikaji wa Kumbukumbu na Uchunguzi wa Ukatili wa Kingono katika Mgogoro* (toleo la 2, 2017), uk, 11. Fasili hii inatumika kwa sababu za kiutendaji na kuakisi kwa sehemu kiini cha Hatua ya Kanuni ya Maadili ya Murad katika *Itifaki ya Kimataifa* iliyotajwa; haijakusudiwa kuzuia matumizi yanayoweza kutokea au umuhimu wa Kanuni ya Maadili ya Murad.

upekee wao (ikiwa ni pamoja na umri, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, dini, utaifa, mbari, hali ya kifamilia) ni msingi wa ujumuishaji ambao ni salama na fanisi.

1.2 **Mazingira Hatarishi ya Kiwango cha Juu:** Tutachukua tahadhari za ziada ambazo ni mahususi kwa ajili ya maslahi mapana ya watoto (inayooana na umri na ukuaji) na kwa wengine ambao huenda wakakabiliana na mazingira hatarishi ya kiwango cha juu na kuzidisha madhara.

1.3 **Kuweka Kipaumbele kwa Wahanga:** Tutaendelea kuweka kipaumbele kwenye haki, mahitaji na matamanio ya mhanga mahususi, kuliko malengo yetu na wakati wote tutaongozwa na usalama wao, ustawi, utu na maslahi mapana.

1.4 **Idhini ya Mhusika:** Tutaheshimu na kuunga mkono uchaguzi wa mhanga. Tutampatia mhanga taarifa kamili, dhahiri, inayoeleweka, isiyoegemea upande mmoja na ya kweli kuhusu uchaguzi uliopo kwa ajili yao, haki na hatari za kuwaruhusu wafanye uchaguzi wao baada ya kupata taarifa za kutosha ama washirikiane nasi au la na kwa masharti gani. Tutakuwa makini kutofanya uchaguzi kwa ajili yao.

1.5 **Kupunguza Shinikizo:** Tutachukua hatua stahikikukabiliana na mambo ambayo yanaweza kuwashinikiza wahanga kuzungumza nasi (kama vile mazingira hatarishi wanayokutana nayo, kutokuwa na usawa katika hadhi au wezo baina yetu, na ushawishi wa jumuiya). Tutawasaidia na kuwezesha fursa zao za kufanya uchaguzi wa kweli, na kubadilisha mawazo yao katika hatua yoyote ikiwa watapenda. Tutaepuka kutengeneza motisha au ushawishi kwa wahanga, au wale wanaowazunguka, ili wazungumze nasi au watu wengine.

1.6 **Vipaumbele vya Mhanga:** Tunakubali kwamba 'haki' (vovyote vile inavyofasiliwa) inaweza isiwe muhimu kwa mhanga husika. Tutaheshimu hii na kuhakikisha hatuathiri vipeumbele vya mhanga au uwezo wao wa kudai haki zoa

1.7 **Kuepuka Ushurutishaji:** Tunatambua kwamba kutumia samansi za lazima au nguvu za kulazimisha kunaweza kuwadhuru wahanga na kunaweza kuwa na matokeo hasi kwenye mchakato wa kutenda haki na matokeo yake.

1.8 **Mgongano wa Maslahi:** Tutachukua muda ili kutambua, kuwa wakweli na wawazi kwetu sisi wenye na kwa wahanga pale ambapo malengo yetu huenda yakagongana na maslahi na haki zao. Hatutaendelea pale ambapo malengo yetu yanagongana.

1.9 **Umiliki:** Tutatambua umiliki wa mhanga wa kisa na uzoefu wao.

1.10 **Kutokuwa na Ubaguzi:** Hatutavumilia au kutenda ubaguzi wowote au tofauti kubwa dhidi ya mtu kwa msingi wa utambulisho wowote, hadhi, sifa, imani, maoni au msingi mwingineo wowote usioruhusiwa

## 2. CHUKUA MUDA, SUBIRI KWANZA

2.1 **Muda na Nafasi ni Muhimu:** Tunatambua kwamba muda wa kutosha na nafasi sahihi ni vipengele muhimu sana kwa ajili ya kushirikiana na mhanga kwa usalama, kimaadili na kwa ufanisi.

2.2 **Kupona Kwanza:** Tunatambua kwamba mchakato wa mhanga kupona ndio unapewa kipaumbele, na kwamba wahanga hawapaswi kushinikizwa au kusukumwa wafichue uzoefu au tukio lolote hadi watakapokuwa tayari kufanya hivyo.

2.3 **Kupunguza Shinikizo la Muda:** Tutatafuta kupunguza shinikizo na ufinyu wa muda ili kusaidia ufanyaji wa maamuzi wa hiari, kupunguza shinikizo kwa wahanga na kuwaruhusu wasimulie kisa chao kwa namna na kwa muda wanaopenda.

2.4 **Mazingira Wezeshi:** Tutaunda mazingira ambayo ni salama kihisia na kimwili kama msingi muhimu kwa ajili ya kufichua na ufanyaji wa maamuzi unaofanywa na waahanga.

2.5 **Faragha:** Tutachagua shehemu ambayo ni ya faragha na ya kipekee kwa ajili ya mahojiano (kwa kushauriana na mhanga pale inapowezekana) na kupunguza hatari za kuonekana, kusikika au kuingiliwa.

2.6 **Kupunguza Idadi:** Tutapunguza idadi ya watu watakaokuwepo wakati wa mahojiano hadi kiwango cha chini kabisa cha lazima na, kadri tutakavyoweza, kuheshimu uamuziwa mhanga kuhusu nani aliyepo (ikiwa ni pamoja na jinsia zao, uhusiano au sababu nyinginezo). Hii hujumuisha iwapo mtu wa usaidizi yupo. Ikiwa hatuwezi kuheshimu uchaguzi wa mhanga tutakuwa na mazungumzo ya uwazi pamoja naye kuhusu sababu na tutaheshimu uchaguzi wake ikiwa ataamua kutoendelea.

2.7 **Mwendelezo:** Pale inapowezekana, tutatafuta kudumisha mwendelezo wa watu wanaowasiliana na wahanga ili kudumisha viwango vya imani na uhuru, na kupunguza hatari ambazo zinawea kutokana na mabadiliko kwa mtu.

2.8 **Usalama na Ubora dhidi ya Idadi:** Tunatambua kwamba mara nyingi kunakuwa na msisitizo usio wa lazima na wenye madhara kuhusu idadi ya mahojiano ya wahanga dhidi ya ubora, na usalama wa ustawi wa wote wanaohusika. Tutaweka kipaumbele katika kutoa mazingira salama na wezeshi na ubora wa maingiliano.

## 3. MAARIFA NA UELEWA WA MAHALI HUSIKA

3.1 **Ufahamu wa Mahali Husika:** Tunatambua kwamba uelewa mzuri wa mazingira ya mahali husika ni muhimu sana na utahakikisha uelewa huu unapatikana ndani ya timu yetu au wale ambao wanatenda kwa niaba yetu Ikiwa sisi si wenyeji wa eneo hilo, tutatafuta kufanya kazi na watendaji wa mahali husika ili tupate ufahamu mzuri wa mzingira hayo.

3.2 **Uelewa wa Kitamaduni:** Tutachukua muda kuelewa namna ambavyo jinsia, umri, hali ya ngono, imani za kidini, kisiasa na imani nyinginezo, hadhi ya kijamii, ulemavu, utambulisho wa kabila na utambulisho mwingineo (sababu zinazoingiliana), zikiwa pamoja na mtazamo na nguvu ya kijamii ya wenyeji huwaathiri wahanga, familia zao, na jumuiya na kazi yetu. Hii hujumuisha pale ambapo mitazamo na nguvu ya kijamii inaweza kuwadhuru wahanga na kuwapatia shinikizo.

3.3 **Sheria na Desturi za Mahali husika:** Tutajifahamisha kuhusu sheria na desturi za mahali husika, na athari zake zinazowezakutoka kwa wahanga na kazi yetu, ikiwa ni pamoja na pale ambapo zinaweza kumhukumu mhanga kwa uhalifu kwa kile kilichotokea au pale ambapo wanalazimisha kutoa ripoti na wajibu wa kufichua. Tutamweleza mhanga haya kabla hajatueleza uzoefu wake, ili aweze kuangalia ikiwa ataendelea au la.

3.4 **Mawasiliano na Maingiliano Stahiki:** Tutafanya kazi ili tuelewe umuhimu na athari ya maneno na maingiliano yetu katika mazingira ya mahali hisika. Tutakuwa makini kubaini mapengo ambayo yanaweza kuweo katika lugha na dhana ya ukatili wa kingono, na tofauti katika desturi za kitamaduni na kijamii ambazo zinaweza kusababisha madhara au jinai.

3.5 **Kupunguza Matokeo Hasi:** Tutatafuta kupunguza matokeo hasi ya kazi yetu katika jumuiya, ikiwa ni pamoja na kuepuka unyanyapaaji, kuwatumia au kuwatia doa wahanga kupitia kushirikiana nasi, au kuufanya mchakato wa kuwabainisha wahanga kuwa wa kibiashara, au kutengeneza au kuzidisha mgogoro au migawanyiko ya kijamii.

3.6 **Watendaji wa Mahali Husika:** Tunatambua jukumu muhimu la watendaji wa mahali husika katika mwendelezo wa usaidizi kwa wahanga na kwa kushughulikia mitazamo hasi kuhusu wahanga katika jamii.

## 4. MAANDALIZI KAMA MSINGI

4.1 **Maandalizi Kwanza:** Tutafanya maandalizi ya kina kabla ya kufanya kazi yoyote na wahanga, kama msingi wa kuheshimu haki za wahanga, na kwa ajili ya matokeo salama, ya kimaadili na yenye ufanisi.

4.2 **Tathmini na Utatuzi wa Hatari:** Tutabainisha na kutathimini madhara yoyote yanayoweza kutokea, hatari au madhara kwa ajili ya wale wote waliohusika ikiwa ni pamoja na usalama wao, ustawi, haki za uchumi wa kijamii na kisheria na kupitia tathmini hii mara kwa mara kadri iwezekanavyo. Tathmini hii itajumuisha hatari zinazoingiliana kwa mtu husika, familia yao na jumuiya. Ikiwa tutaendelea kuwasiliana na mhanga, tutawomba kubainisha dukuduku zao, kama sehemu ya tathmini ya hatari inayoendelea. Tutachukua hatua stahiki ili kushughulikia hatari hizo na kuhakiki hatua hizi mara kwa mara kadri iwezekanavyo. Hatutaendelea ikiwa hatari hizo haziwezi kutatuliwa vizuri.

4.3 **Kuweka Katika Muktadha Ukatili wa Kingono:** Tunatambua kwamba ukatili wa kingono hautokei vivi hivi. Ufichuaji wa ukatili wa kingono unaweza kutokea bila kutarajia. Tutajiandaa kwa ajili ya uwezekano huo na kuweka mipango stahiki. Pia tutasikiliza ikiwa mhanga anachagua kuzungumzia kuhusu uhalifu mwingineo, tukitambua kwamba huenda wakawa wamestahimili hatari na shida nyinginezo.

4.4 **Ubainishaji wa Mtendaji:** Tutafanya kazi ya kumbaini mtendaji ili kuwaelewa watendaji wote stahiki, ikiwa ni pamoja na nani anakusanya taarifa kutoka kwa wahanga kwa kusudi gani, na kutusaidia kuwa na uelewa wa kuongeza thamani chini ya Kanuni ya 5.

4.5 **Kubainisha Njia za Rufaa:** Tutabainisha huduma za usaidizi na mifumo kwa ajili ya wahanga, ambayo inafikika, salama, ya siri, yenye ufanisi, na inayozingatia umri na jinsia, ikiwa ni pamoja na huduma za matibabu, afya ya akili na saikolojia ya kijamii, ulinzi na sheria. Tutajitahidi kutambua na kupunguza vikwazo vya kufikia usaidizi kwa ajili ya wahanga wakati wowote inapowezekana.

4.6 **Uratibu na Ushirikiano:** Tunatambua umuhimu mkubwa wa uratibu na ushirikiano, kwa ajili ya kuepuka madhara, kuwaweka wazi wahanga kupita kiasi na athari katika haki zao kupitia kazi yetu, na tutawasiliana na wale ambao wanafanya kazi katika sehemu moja ili kutafuta njia za kufanya kazi pamoja kwa ajili ya matokeo bora ya mhanga.

4.7 **Ufuatiliaji:** Tutapanga na kufanya kadri tuwezavyo kuendelea kuwasiliana na wahanga ili kuwapatia mrejesho kuhusu matokeo ikiwa wanakubali matokeo hayo, kuwezesha mapitio ya idhini ya mhusika ikwa na pale ambapo ni lazima. Ikiwa hatutaendelea kukaa mahali husika, tutawaomba washirika wanaokaa mahali husika watusaidie.

## 5. ONGEZA THAMANI AU USIFANYE

5.1 **Kusudi Dhahiri:** Tutakuwa na uwazi kwenye kusudi na wajibu wetu, kwa nini tunakusudia kukusanya taarifa kutoka kwa wahanga, na vile tutakavyotumia taarifa zilizokusanywa.

5.2 **Matokeo Yenye Uhalisia:** Tutaendelea tu pale ambapo kusudi letu linaweza kufikiwa kwa uhalisia kwa kutumia rasilimali zetu, muda na ujuzi, bila kusababisha madhara zaidi,

5.3 **Vyanzo Mbadala:** Tutatafuta vyanzo mbadala vya taarifa (kwa wahanga wote, hasa kuhusu watoto, na ambapo kuna hatari ya kiwewe, madhara au athari kwa haki za mhanga), na tutajiuliza iwapo mamlaka au kusudi letu kweli linahitaji hatari ya kuwafuata wahanga.

5.4 **Uzingatiaji wa Ongezeko la Thamani:** Kabla ya kuamua kuendelea, tutatafakari kwa uaminifu juu ya kile ambacho ongezeko la thamani au manufaa yanayoweza kuletwa na kazi au vitendo vyetu kwa mhanga husika. Tutamfuata mhanga ikiwa tu kuna ongezeko la thamani la kweli, lisiloegemea upande mmoja kutokana na kazi yetu.

5.5 **Kupunguza Kuonekana:** Tunatambua kwamba mahojiano mengi yanaweza kusababisha kiwewe na yanaweza kutengeneza kumbukumbu ambazo si linganifu au si sahihi ambazo zinaweza kukwamisha haki za mhanga, ikiwa ni pamoja na kupata haki au fidia. Tutajitahidi sana kupunguza kuonekana huku.

5.6 **Kushiriki Taarifa:** Tutajadili na mhanga uwezekano wa kushiriki maelezo/kumbukumbu za mahojiano na watendaji wengine wanaoaminika ili kuepuka urudufishaji wowote usio wa lazima au kuwekwa katika kiwewe zaidi au hatari nyinginezo. Kushiriki taarifa kwa aina yoyote ile kunapaswa kutathminiwa hatari. Pale ambapo tunaweza kushiriki taarifa kwa usalama na mhanga amekubali, tutafanya hivyo.

5.7 **Mahojiano ya Kabla:** Tutachukua hatua wakati wa maandalizi ili kujua iwapo mhanga amehojiwa hapo kabla na badala yake kufanya jitihada za kupata na kutumia kumbukumbu zilizopo (ikiwa mhanga amekubali). Tutamuuliza tena mhanga kabla ya kuanza mahojiano yoyote.

5.8 **Mtaarifu Mhanga Kuhusu Hatari za Urudufishaji:** Pale ambapo mahojiano ya ziada yataongeza thamani halisi na kweli inahitajika kwa ajili ya kazi yetu, tutaelezea faida na hatari za kufanya mahojiano tena na kuwapatia nafasi na muda ili waamue ikiwa wapo tayari kuchukua hiyo hatari. Ikiwa watachagua kuendelea, tutakuwa mahususi na tuliokusudia katika mbinu zetu za kuongeza hilo ongezeko la thamani na kupunguza hatari za kufanya tena utafiti.

## 6. MIFUMO, UMAHIRI NA UENDELEZAJI

6.1 **Umahiri, Ujuzi na Mitazamo:** Tutawafuata wahanga pale tu ambapo tumechukua hatua ili kuhakikisha ujuzi wa lazima, umahiri na mitazamo ndani ya timu yetu (ikiwa ni pamoja na wapatanishi, wakalimani na wengineo wanaofanya kazi kwa niaba yetu), mashiko ya mbinu zetu. Hizi hujumuisha: uanuwai, mtoto, umri na uwezo unaofaa mambo nyeti; jinsia na kutambua muktadha wa mahali husika; ukatili wa kingono na unyanyapaaji; ujuzi wa kufanya usaili; na uelewa wa msingi wa kiwewe na ufahamu,

6.2 **Miongozo ya Kiufundi na Viwango:** Kama itakavyolazimika, tutachukua muda ili kuendeleza zaidi ujuzi huu, kuelewa miongozo ya kiufundi inayohusika, na kushauriana na wataalamu.

6.3 **Kikomo cha Utaalamu:** Tutakuwa wakweli, na kubaki ndani ya mipaka ya ujuzi wetu na ufahamu wa muktadha. Tutatambua uwezo wetu na mipaka yetu.

6.4 **Kumhoji Mhanga Mtoto:** Ni wale tu wenye mafunzo na uzoefu mahususi wanaofanya kazi na watoto (mahususi kwa umri, ukuaji na mahitaji) ndio watakaowafanyia usaili wahanga watoto.

6.5 **Usaidizi na Mwitikio Stahiki:** Kufuatia ubainishaji wetu wa huduma ya usaidizi chini ya Kanuni ya 4, tutaendelea tu ikiwa kuna angalau usaidizi wa msingi na mwitikio ili kushughulikia madhara ya kisaikolojia yanayowezakutokea kutokana na kazi yetu, mahitaji ya haraka ya kitabibu, saikolojia ya jamii au ulinzi ambayo yanapaswa kushughulikiwa

kabla ya mahojiano. Ikiwa hakuna usaidizi au mwitiko huo tunapaswa kufikiria usadizi wa mara moja moja au wa masafa au (kuruhusu muda kwa ajili ya) kuunda kwanza uwezo unaohitajika kabla ya kuendelea.

6.6 **Ulinzi wa Usiri:** Tutaweka itifaki za usiri na hatua za kulinda taarifa na data za mhanga, ikiwa ni pamoja na kuwa waangalifu ili kuhakikisha ulinzi wa mawasiliano yoyote ya mtandaoni, usimamizi na uhifadhi wa data. Hii inategemeana na uchaguzi wa wazi na mahususi wa mhanga kuhusu ni nani wa kushiriki naye taarifa, na ukomo wowote wa kisheria na ukomo mwingineo unaoweza kutumika kuhusiana na usiri.

6.7 **Maelekezo:** Tutawaelekeza timu yetu na wale ambao wanafanya kazi kwa niaba yetu (ikiwa ni pamoja na washirika wowote) kuhusu michakato na itifaki salama, za kimaadili na zenye ufanisi.

## 7. MAHOJIANO YA HESHIMA NA SALAMA

7.1 **Tathmini kabla ya Kuwafikia:** Kulingana na mazingatio ya msingi kwenye Kanuni hii ya Maadili, tutatathmini kwa uangalifu wakati gani wa kuwafikia na wakati gani si wa kuwafikia wahanga kwa ajili ya taarifa. Ikiwa hatuwezi kuendelea kwa usalama au kwa kuzingatia Kanuni hii ya maadili, basi hatutaendelea wakati huu. Baada ya kuwa tumekutana na mhanga, tutafanya uamuzi wowote pamoja na mhanga kama sehemu ya mazungumzo ya wazi kwa kuzingatia Kanuni ya 1.

7.2 **Kuwa Makini na Kiwewe:** Tutahakikisha timu yetu imepata mafunzo ili kutambua dalili za kiwewe na mfadhaiko, jinsi ya kupunguza uwezekano wa athari za kusababisha kiwewe kutokana na mwingiliano na jinsi ya kuchukua hatua za msingi ili kumsaidia mhanga ikiwa hii inatokea.

7.3 **Utu na Heshima:** Tutawatendea wahanga kwa utu na heshima kama wanadamu, na kwa huruma, kujali, heshima na kuthamini.

7.4 **Uchunguzi:** Pamoja na tahimini ya hatari katika Kanuni ya 4, mwanzoni mwa mahojiano pia tutachunguza tena masuala ya usalama, hatari nyinginezo, faragha, na ustawi/hali ya kihisia ya mhanga, mapengo yoyote katika kuelewa na kuwasiliana, na shinikizo lolote kwa mhanga ili aendelee.

7.5 **Kueleweka:** Tutawasiliana kwa lugha na maneno ambayo mhanga anaelewa (ikiwa ni pamoja na kutumia umri, jinsia, uwezo na lugha inayofaa kulingana na utamaduni). Hili ni jambo muhimu sana kwa ajili ya mazunguzo ya uwazi na heshima, na machaguo yanayofanywa na wahanga.

7.6 **Uwakilishi wa Haki na Sahihi:** Pia tutahakikisha kuwa tunaweza kumwelewa mhanga, ili tuwe na uwakilishi wa haki na sahihi juu ya kile wanachotamani kusema. Tutahakikisha kiwango hiki cha mawasiliano kabla ya kuendelea.

7.7 **Muundo wa Mahojiano Salama:** Tutahakikisha kwamba mahojiano yetu yana muundo salama na nyeti. Tutatafuta kuweka muktadha wa unyanyasji wa kingono dhidi ya uzoefu mpana , hatutawekea mkazo kwenye, kujohi au kuchukua maelezo ya wazi au katika picha ya ukatili wa kingono kutoka kwa mhanga. Pia tutakuwa waangalifu tusitoe taarifa ya ukatili wa kingono kwa namna hiyo.

7.8 **Maswali ya Wazi:** Tutatumia maswali ya wazi, na kuyafanya maswali yetu yawe katika kasi, kiwango na toni ya kadri. Kwa kutambua athari inayowezakutokea ya maswali funge au ongozi kwa mhanga na juu ya usahihi wa taarifa iliyokusanywa kwa namna hiyo, tutakuwa na kikomo cha maswali hayo isipokuwa tu kwa mazingira mahususi.

7.9 **Ufungaji Salama:** Tutachukua muda wa kufunga mahojiano kwa uangalifu na namna salama, tukimrejesha mhanga katika wakati uliopo, na kutambua muda wao na ujasiri wa kusimulia kisa chao. Tutajadiliana na mhanga juu ya mawasiliano ya ufuatiliaji kwa kuzingatia Kanuni ya 4.

## 8. UADILIFU NA UWAJIBIKAJI

8.1 **Kutonyanyapaa**: Tutachunguza na kupambana na upendeleo wetu, woga, mitazamo na makisio kwa kuhusiana na ukatili wa kingono na wahanga wa ukatili wa kingono. Hatutatoa ujumbe wowote kwa wahanga (kupitia maneno, lugha ya mwili au matendo) ambayo yanalaumu, aibisha, kuwadhuru au kutowaheshimu.

8.2 **Kutokuwa Wanyonyaji:** Hatutakuwa wachimbuaji, kuwatumia, kunyonya, kunyanyasa au kutumia fursa ya unyonge wa wahanga.

8.3 **Ukweli na Unyofu:** Tutakuwa wakweli, wawazi na halisi kwa wahanga kuhusu kazi yetu, matokeo yake na hatari zinazoweza kutokea. Tutawauliza wana matarajio gani, na kuhakikisha tunakuwa na uhalisia katika kutoa taarifa kuhusu kile tunachoweza na ambacho hatuwezi kufanikiwa au kutoa.

8.4 **Kuaminika:** Tunatambua umuhimu wa kuaminika. Hatutatoa ahadi mbazo huenda tusizitimize au ambazo hatuwezi kuzitimiza. Tutafuatilia ahadi zozote tunazozitoa kwa wahanga.

8.5 **Kupata Haki:** Tutaiheshimu haki ya mhanga ya kutafuta tiba yenye ufanisi, ikiwa ni pamoja na kupata haki, fidia na mianya mingine ya kisheria ili kulinda haki zao. Tunatambua kwamba kumbukumbu au ripoti za mahojiano huenda zikatumika dhidi ya wahanga, ikiwa ni pamoja na wale ambao wamehusika katika ukiukaji na mahakamani au michakato mingineyo.

8.6 **Hakuna Upotevu wa Ushahidi:** Hatutachukua au kuondoa nyaraka halisi, vitu vya kushikika au ushahidi mwingineo kutoka kwa mhanga au mahali fulani, hata pale ambapo tumeombwa kufanya hivyo, isipokuwa kama tuna mamlaka, ni lazima, tunaweza kufanyha hivyo kwa usalama, na iwapo tuna uwezo wa kusimamia na kuhifadhi ushahidi huo.

8.7 **Kiwewe cha Pili:** Tutahakikisha hatua zinachukuliwa ili kupunguza kiwewe chetu na athari mbaya za kazi tunayoifanya na timu yetu, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya msingi kuhusu ishara na dalili za kiwewe cha pili, itifaki za usaidizi na mbinu salama za kufanya kazi ikiwa ni pamoja na ulinzi juu ya ujazo au aina ya kazi.

8.8 **Ulalamikaji na Uwajibikaji:** Tutatumia mifumo iliyopo, au pale ambapo ni lazima kufanya kazi na washirika ili kusaidia kutengeneza, kufuatilia mawasiliano ya mrejesho kwa ajili ya malalamiko ya mhanga, na malalamiko yanayotolewa na watoa huduma au wengineo kuhusu kitendo ambacho kinavunja Kanuni hii ya Maadili.

**KIAMBATISHO B: MIFANO YA VYANZO VYA UTAFITI USIO WA MKATABA KWA AJILI YA UTENGENEZAJI WA RASIMU YA KANUNI YA MAADILI YA MURAD**

*Marejeo kamili yakiwa na nukuu kamili yatachapishwa pamoja na tangazo.*


1. EU, Directive 2012/29/EU Minimum Standards on the Rights, Support and Protection of Victims of Crime, 25 Oct 2012
2. UN, ECOSOC Guidance on Justice Matters involving Child Victims and Witness of Crimes
3. UN, Basic Principles and Guidelines on the Right to a Remedy and Reparations for Victims of Gross Violations of International Human Rights Law and Serious Violations of International Humanitarian Law (A/RES/60/147)
4. UN, Declaration on Basic Principles of Justice for Victims of Crime and Abuse of Power (A/RES/40/34)
5. UN, Comprehensive Strategy on Assistance and Support to Victims of Sexual Exploitation and Abuse by United Nations Staff and Related Personnel (A/RES/62/214)
6. UN, Guidance Note of the UN Secretary-General, Reparations for Conflict-Related Sexual Violence (June 2014)
7. OHCHR, Manual for Human Rights Monitoring
8. OHCHR, Commissions of Inquiry and Fact-Finding Missions on International Human Rights and Humanitarian Law Guidance and Practice (2015)
9. WHO, Ethical and Safety Recommendations on Sexual Violence in Emergencies
10. WHO, Ethical and Safety Recommendations on Domestic Violence Research
11. WHO, Guidelines for Medico-Legal Care for Victims of Sexual Violence (2003)
12. WHO, Ethical and Safety Guidelines for Interviewing Trafficked Women (2003)
13. Researching Violence Against Women: A Practical Guide for Researchers and Activists (WHO & PATH, 2005)
14. UNFPA, Minimum Standards for GBV Interventions (2017)
15. UNFPA, Reporting GBV in the Syria Crisis, A Journalists Handbook
16. Inter-Agency Minimum Standards for Gender-Based Violence in Emergencies Programming (GBVMS) (2019)
17. UNHRC, Regional Safe Spaces Network and UC Berkeley School of Law HRC, THE SILENCE I CARRY Disclosing gender-based violence in forced displacement, Guatemala & Mexico, Exploratory Report 2018
18. UNHRC and Refugee Law Project, Working with Men and Boy Survivors of Sexual and Gender-Based Violence in Forced Displacement, Need to Know Guidance 4 (2012)
19. IASC, GBV Guidelines (updated 2015)
20. IASC, GBV Guidelines Companion Pocket Guide: How to Support Survivors of Gender-Based Violence When a GBV Actor is Not Available in Your Area: A Step-By-Step Pocket Guide for Humanitarian Practitioners (2015)
21. IASC Guidelines, Inclusion of Persons with Disabilities in Humanitarian Action (2019)
22. Gender-based Violence Information Management System, Inter-Agency Gender-Based Violence Case Management Guidelines: Providing Care and Case Management Services to Gender-Based Violence Survivors in Humanitarian Settings (1st ed, 2017)
23. GBV AoR, Handbook for Coordinating Gender-Based Violence Interventions in Emergencies (2019)
24. GBV Global Protection Cluster, Media Guidelines for Reporting on Gender-Based Violence in Humanitarian Contexts
25. UNODC and UNICEF, United Nations Guidelines on Justice in matters involving child victims and witnesses of crime
26. UN Action, Reporting and Interpreting Data on Sexual Violence from Conflict-Affected Countries, The “Dos and Don’ts” (2008)
27. UN Office of the Victims’ Rights Advocate, Draft Statement on Victims’ Rights (2019 draft, internal)
28. UN Office of Victims’ Rights Advocate, Report from Expert Workshop on Victims’ Rights, UNHQNY, (30-31 May 2019) (internal)
29. ICC, Office of the Prosecutor, Policy on Children (November 2016)
30. ICC Code of Conduct for Prosecutors
31. ICC Code of Conduct for Investigators
32. STL, Practitioner's Handbook on Defence Investigations in International Criminal Trials (2017)
33. African Commission on Human and Peoples’ Rights Guidelines for Combatting Sexual Violence and its Consequences in Africa (Naimey Guidelines) (2017)
34. OSCE ODIHR, Preventing and Responding to SGBV in Detention (2019)
35. ICRC, Professional Standards for Protection Work (2018)
36. Child Protection Working Group, Minimum Standards for Child Protection in Humanitarian Action (CPMS) (2019)
37. The Sphere Handbook: Humanitarian Charter and Minimum Standards in Humanitarian Response (2018)
38. American Sociology Association Code of Ethics

39. British Psychology Society Code of the Ethics and Conduct, including Code of Research Ethics
40. World Medical Association Helsinki Declaration of Ethical Principles on Research with Human Subjects
41. International Ethical Guidelines for Health Research with Humans
42. RESPECT Code of Socio-Economic Research
43. Council for International Organizations of Medical Sciences (CIOMS), International Ethical Guidelines for Health-related Research Involving Humans (4th ed, 2016)
44. Charter on Inclusion of Persons with Disabilities in Humanitarian Action (2016)
45. NATO Provisional Guidance Note on Implementation of Security Council Resolution 1960 (2010) on Women, Peace and Security (Conflict Related Sexual Violence) June 2011, Annexes 2016
46. General Principles for Obtaining the Best Evidence from Vulnerable Witnesses to Sexual and Gender Based Violence Offences Pilon SGBV Working Group (Pacific Islands Law Officers Network) (2017)
47. New Zealand Victim's Code
48. Iowa State Sexual Assault Victims Advocate Code of Ethical Conduct
49. Saferworld: Research in Conflict Settings – Gender and Ethics
50. Health and Human Rights Info (HHRI), Mental health and gender-based violence: Helping survivors of sexual violence in conflict – a training manual (2014)
51. International Protocol on Investigation and Documentation of Sexual Violence in Conflict (2nd ed, 2017)
52. Istanbul Protocol: Manual on the Effective Investigation and Documentation of Torture and Other Cruel, Inhuman or Degrading Treatment or Punishment, Professional Training Series No. 8/Rev.1 (under review)
53. U.S. Department of Justice, Office on Violence Against Women, A National Protocol for Sexual Assault Medical Forensic Examinations Adults/Adolescents (2nd ed, 2013)
54. Global Rights Compliance Basic Investigative Standards for First Responders (2019)
55. PILPG, Handbook on Civil Society Documentation of Serious Human Rights Violations: Principles & Best Practices (2016)
56. Human Rights Watch, Interview Manual (internal, not public) (2019)
57. Guidelines on International Human Rights Fact-Finding Visits and Reports by Non-Governmental Organisations (The Lund-London Guidelines) (2015)
58. AJAR, Manual for Rebuilding Lives and Communities after Torture (2017)
59. AJAR, Stone and Flower: A Guide to Understanding and Action for Women Survivors (2nd ed, 2017)
60. Dart Centre, Tip-sheet for Sexual Violence Reporting & Tragedies Reporting Guidelines
61. Women' Media Centre, 10 do's and don'ts on how to interview sexualised violence survivors (2017)
62. Mookherjee, Nayanika, Guidelines Towards Ethical Testimonies of Sexual Violence during Conflict. University of Durham (2019)
63. B von der Lippe & R Ottosen (eds.), Gendering War and Peace Reporting: Some Insights – Some Missing Links, Nordicom (2016)
64. R Campbell, Training Interviewers for Research on Sexual Violence: A Qualitative Study of Rape Survivors' Recommendations for Interview Practice, Violence Against Women (March 2009)
65. J Foster & S Minwalla, Voices of Yazidi women: Perceptions of journalistic practices in the reporting on ISIS sexual violence, Women's Studies International Forum 67:53-64 (March 2018)
66. P Bouvier, Sexual violence, health and humanitarian ethics: Towards a holistic, person-centred approach, International Review of the Red Cross (2014), 96 (894), 565–584.